



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**  
**(MAMLAKA YA MJI MDOGO WA HAI)**  
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*



**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 27-29 74369

Fax : 27-29 74368

Email: [ded@haidc.go.tz](mailto:ded@haidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Mamlaka ya Mji Mdogo

S.L.P 27

**HAI**

**Kumb.Na.LG/D.30/18/1/38**

**Tarehe: 23.02.2022**

**TANGAZO LA ZABUNI**

1. Mamlaka ya mji mdogo wa Hai kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hai inatangaza Zabuni ya ukusanyaji na uzoaji taka katika maeneo/mitaa yote ya mji mdogo wa Hai. Zabuni hii ni pamoja na ukusanyaji wa ada na tozo kwa kuzingatia sheria ndogo ya mazingira ya mwaka 2016 na marekibisho yake ya mwaka 2020.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inapenda kuwaalika watu binafsi, ushirika, makampuni, taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria vyenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hii kutuma maombi yao kwa zabuni ifuatayo:
3. Muombaji anapaswa kuwasilisha ombi lake akiambatisha stakabathi ya malipo ya Tshs. 50,000/= kama ada ya maombi, ambayo haitarudishwa (non-refundable fee).
4. Kitabu cha zabuni (Bidding Document) chenye masharti ya zabuni kinapatikana kwenye Ofisi ya Mtendaji Mamlaka ya Mji mdogo Hai siku za kazi baada ya kuonesha stakabathi ya malipo. Katika barua ya maombi ni lazima muombaji ambatishe maoteo na mchanganuo wa kiasi ambacho muombaji atawasilisha Halmashauri.
5. Zabuni ziwe nakala tatu (3), halisi moja na nakala zingine mbili zifungwe vizuri katika bahasha ya A4 kwa lakiri (wax) na kuandikwa aina ya zabuni, namba ya zabuni, kila zabuni iwe katika bahasha yake na kisha zote ziwekwe katika bahasha moja na maombi yatumwe kwa Mtendaji - Mamlaka ya Mji mdogo Hai S.L.P 27 HAI
6. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa pamoja na zabuni zitakazotumwa kwenye mtandao (E-mail) hazitapokelewa.
7. Mwombaji ni lazima awe na vitendea kazi vifuatavyo:-
  - a) Magari maalumu ya kubebea taka
  - b) Awe na vifaa vya kukusanyia taka
  - c) Awe na raslimali watu wa kutosha
8. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya Jumanne tarehe 01/03/2022 saa 09:30 Alasiri na ufunguzi utafanyika hadharani katika Ukumbi wa Halmashauri mara tu baada yakufunga kupokea zabuni.
9. Kwa mahitaji ya ufafanuzi wowote fika Ofisi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri siku za kazi.

Dionis M. Myinga

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**HAI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W.**

**HAI**